# Madarasa bila Kuta

CHUNGUZA – GUNDUA – JIFUNZE – PENDA


## Watoto wa popo

Somo

5

**Tutajifunza nini wiki hii:**

- Kwa nini ni kazi ngumu sana kuwa popo mama
- Maskani ya uzazi ni nini
- Ni nini hufanya maskani iwe mzuri kwa uzazi
- Ni nini popo mchanga lazima ajifunze kuishi



Hi ni Spike hapa. Somo hili linahusu popo wachanga, lakini kwa sababu mimi ni mwanamume si jambo ninalolijua sana. Popo baba hawasaidii kuchunga popo watoto. Kwa hivyo ninawapa wataalam fursa hii.



Hujambo mimi ni Saba, unaweza kunijua kama popo wa Dingan, kwa kimombo African yellow house bat, popo wa nyumbani mwenye tumbo la manjano au popo wa nyumba ya manjano ya Kiafrika. Nina watoto mapacha, wananijua tu kama "mama"!



Habari, mimi ni Bongi. Mimi ni popo aina ya Botswanan brown long-eared bat. Mimi ni mama mwenye fahari sana wa mtoto Logan. Kutunza mtoto mmoja ni kazi ngumu sana sijui jinsi Saba anavyoweza na wawili.

Usisahau, ishara ya penseli inamaanisha kuwa ni zamu yako kufanya shughuli!
Tumejumuisha maneno yote mapya katika orodha ya maneno mwishoni!

**Utahitaji:**

- penseli
- kikokotoo

## 1 Akina mama popo ndio wabora zaidi!

Mwishoni mwa majira ya kuchipua, nyakati za usiku zinapokuwa na joto na kunapokuwa na chakula cha kutosha, mama popo huanza kujiandaa kupata watoto wao. Kwanza lazima watafute mahali penye joto na salama pa kukaa, mahali palipo karibu na chakula kizuri. Hii itakuwa maskani yao ya uzazi.




Hapa ndipo watakapojihifadhi;

- wakiwa wajawazito,
- watakapo jifungua,
- na ambapo wanamtunza mtoto wao hadi yuko; kubwa vya kutosha kuruka, kuweza kupata chakula chake na kuishi bila mama yake.

## 2 Maskani ya uzazi/Kitalu




Mahali panapotumiwa na akina popo mama na watoto huitwa maskani ya uzazi au kitalu. Mara tu popo wanapokuwa wamepata maskani mazuri ya uzazi watajaribu kurejea humo kila mwaka ili kupata mtoto wao mwingine.

Popo wa kike atarudi mahali ambapo yeye mwenyewe alizaliwa anapotarajia mtoto wake (ikiwa bado ipo). Inawezekana kwamba atampata mama yake mwenyewe, nyanya, nyanya mkuu na shangazi zake wengi pia wamerudi kwenye makao hayo, kila mmoja akitarajia mtoto pia.


Ikiwa kiota cha uzazi kitapotea, kwa mfano mti ukianguka, jengo libomolewe au pango lenye utulivu liwe na kelele kwa sababu ya utalii, popo mama lazima watafute kitalu kipya. Kukipata kitalu kilicho na hali zinazofaa, (joto, salama na karibu na chakula) kunaweza kuwa vigumu na kufanya maisha kuwa magumu zaidi kwa popo wajawazito.

Chumba cha uzazi kitakuwa na wanawake wazima (popo mama) na watoto wa kiume na wa kike/popo wachanga. Wanaume wazima hawasaidii kutunza watoto na wanaishi katika maskani tofauti.





# Shughuli 1:
# Je, ni akina mama na popo wangapi unaweza kuhesabu kwenye picha hii?

Katika maskani hii ya mti kuna akina mama wengi pamoja na watoto wao, wakikumbatiana kwa uzuri na joto. Ni akina mama wangapi (macho makubwa) na watoto (macho madogo) unaweza kuhesabu?







Bats without Borders.org

# 3 Mimba / Ujauzito

Popo wadogo (kama Bongi na Saba) huwa na mimba kwa wiki 6 hadi 9. Huu ni muda mrefu kwa mamalia mdogo kama huyo. (Panya huwa mjamzito kwa takriban wiki tatu.)

Muda ambao mnyama ana mimba huitwa kipindi cha ujauzito.
Popo wa kike aliyekomaa na mwenye afya njema kwa kawaida atakuwa na mtoto mmoja kwa mwaka. Aina fulani za popo wana mapacha, lakini hii ni maalum kidogo. Spishi nyingi zina mtoto mmoja tu.



Nilijua nilikuwa maalum. Kupata mapacha ni jambo lisilo la kawaida!



Kweli, kupata mtoto mmoja baada ya mwengine inanitosha mie!

Lakini sisi sio kama mamalia wenzetu, panya, ambaye ana watoto wengi mara kadhaa kwa mwaka! Hapana, Asante!!



Bats without Borders.org

# 4 Popo watoto wakati wa kuzaliwa



Ni lazima iwe kazi ngumu sana kwa popo mama kuzaa. Mtoto anapozaliwa ni mkubwa sana ukilinganisha na saizi ya mama yake.



"Logan alikuwa na gramu 2.5 alipozaliwa, inaweza isisikike kuwa mzito sana kwako lakini nilikuwa na uzito wa gramu 7 tu kabla ya kuwa mjamzito. Alikuwa zaidi ya theluthi moja ya uzito wangu wa kawaida!"


"Nilikuwa na gramu 50 nilipozaliwa, hiyo ilikuwa karibu sehemu ya sita (1/6) ya uzito wa kawaida wa mama yangu (gramu 300). Wakati nilipoachishwa kunyonya nilikuwa na uzito wa gramu 135."






## Shughuli 2: Uzito wa mtoto

Unaweza kutaka kujua ni sehemu gani ya uzito wa mama yako ulikuwa wakati wa kuzaliwa.



Ili kufanya hivyo, gawanya uzito wa kawaida wa mama yako (kabla ya kuwa mjamzito) na uzito wako wa kuzaliwa. (Pengine ni rahisi kufanya kazi kwa kilo badala ya mawe, paundi na ounces). Kisha weka jibu lako chini ya 1. Kwa mfano, ikiwa uzito wa mama ukigawanywa na uzito wa mtoto = 19, sehemu ni 1\19.

**Jibu:**


Ikiwa mama yako hakumbuki hapa kuna mfano:
Uzito wa mama kabla ya ujauzito = 60Kg
Uzito wa mtoto wakati wa kuzaliwa = 3kg

## 5 Shikilia tu hapo mtoto!

Watoto wa popo huzaliwa wakiwa hoi sana, macho yao yamefungwa, hawana manyoya lakini wanajua jinsi ya kuning'inia kwa mama yao mara moja. Watashika kwenye chuchu yake kwa midomo yao na kushikilia mwili wake kwa vidole vyao. Kwa njia hiyo wanalishwa, joto na kuingizwa salama.



## 6 Kulisha na kupaa



Mwanzoni, mama na mtoto hutumia wakati wao wote pamoja. Mtoto hula maziwa kutoka kwa mama yake. Mama lazima awe na uwezo wa kujilisha vizuri ili kutengeneza maziwa mengi kwa mtoto wake anayekua. Hii ina maana kwamba mama lazima aondoke kwenye kiota ili kujilisha.

Mama anaweza hata kupaa na mtoto wake akiwa amemshikilia. Anaweza kupaa hivi kwa kawaida hadi mtoto wake anapokuwa na umri wa wiki moja au na popo wa matunda hadi mtoto awe karibu theluthi moja ya uzito wake. Baada ya hapo, atamfanya popo mtoto amngojee na watoto wengine wote kwenye koloni, ili wajiweke joto wakati anaenda kuwinda. Popo mama mmoja anaweza kubaki nyuma ili kuwaweka salama, lakini akina mama watakuja na kwenda usiku kucha kuwalisha watoto wao maziwa.
Wakati mama anarudi kwenye maskani ya uzazi atamtambua mtoto wake katika koloni kwa kilio chake na harufu yake.





Bats without Borders.org




# Shughuli 3:
# Linganisha mama na mtoto wake

Je, unaweza kulinganisha mtoto wa popo na mama yake? Fuata mistari kuona nani ni wa nani!




# 7 Kukua ni kitu ngumu kufanya

Watoto wa popo wana mengi ya kujifunza, wanapaswa kujifunza;

jinsi ya kuruka,



jinsi ya kupata chakula (kunusa matunda yaliyoiva, chavua au nekta au kuwinda mawindo hai).



Kwa baadhi ya popo kutafuta chakula kunamaanisha pia kukipata, (Logan lazima ashike nondo na wadudu wengine, fikiria kujaribu kuruka na nondo anayeng'ng'ana kukutoka mdomoni au kwenye mguu wako),

na popo wengi wanahitaji kujifunza jinsi ya kutoa mwangwi! (Popo wa matunda hawatoi mwangwi lakini wengine wote hufanya hivyo).

Yote haya katika wiki 4 hadi 6, ambayo ni wakati wa kawaida inachukua popo mtoto kuondoka maskanini. Baadhi ya popo wachanga hujifunza jinsi ya kupaa kwa kumshika mama, na kupeperusha mabawa yao juu chini.

Mara tu wanapojifunza kupaa kuna ujuzi mwingi zaidi wanaohitaji...

## Ujuzi unaohitajika:

- kuepuka kuwindwa,
- jinsi ya kupata njia ya kurudi nyumbani,
- jinsi ya kuzunguka mahali wanapoishi,
- ambapo kuna maskani mengine ya kujikinga,
- jinsi ya kuokoa nishati (kwa kwenda torpid) wakati chakula ni chache.



Mwaka wa kwanza wa maisha ya popo ni ngumu sana, kuna mengi ya kujifunza! Nadhani nitalala tu kwa sasa! Usiku mwema!

# Faharasa
# (maneno ambayo tumejifunza leo!)

**Ujauzito** - ni wakati ambao mtoto huchukua kukua ndani ya mama yake hadi awe tayari kuzaliwa. (Wakati mama ni mjamzito.)

**Koloni wa uzazi** – kundi la popo wa kike wanaokaa pamoja wakiwa wajawazito, wakizaa na kuwatunza watoto wao.

**Maskani ya uzazi** - mahali panapotumiwa na popo wa kike wakiwa wajawazito, wakijifungua na kuwatunza watoto wao. Nyumba nzuri ya uzazi inapaswa kuwa ya joto, salama (kutoka kwa wanyama wanaowinda popo au usumbufu) na karibu na maeneo mazuri ya kulisha.



Natumai umejifunza mengi leo!
Tukutane wiki ijayo, ili kujifunza yote kuhusu vipeperushi vya kupendeza!

Usisahau; suluhu za shughuli zitapatikana kwenye ukurasa wa Facebook wa Bats Without Borders!

BatsWithoutBorders.org